# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA




# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TANO

## KIKAO CHA NANE

**05 NOVEMBA, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TANO

## KIKAO CHA NANE – TAREHE 05 NOVEMBA, 2026

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA KILIMO:**

Maelezo ya Waziri wa Kilimo kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kimataifa wa Sukari wa Mwaka 1992 *(International Sugar Agreement of 1992).*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kimataifa wa Sukari wa Mwaka 1992 *(International Sugar Agreement of 1992).*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Maelezo ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari juu ya Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Tanzania Kujiunga na Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Usalama wa Angamtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2014 (Mkataba wa Malabo).

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu juu ya Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Tanzania Kujiunga na Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Usalama wa Angamtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2014 (Mkataba wa Malabo).

## III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

## IV. MASWALI YA KAWAIDA:

## OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

**113. MHESHIMIWA MARTHA NEHEMIA GWAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Wodi za kulaza Wagonjwa katika Kituo cha Afya Kintinku.

**114. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya Kata za Swaya na Bujela katika Jimbo la Rungwe.

**115. MHESHIMIWA PROF. PIUS ZEBHE YANDA (BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya kwenye Kata 11 kati ya 20 katika Jimbo la Buhigwe.

**WIZARA YA NISHATI:**

**116. MHESHIMIWA SARA MSAFIRI ALLY (MVOMERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Gridi 220/33KV na ujenzi wa Laini ya 220KV eneo la Dumila Jimbo la Mvomero.

**WIZARA YA KILIMO:**

**117. MHESHIMIWA MOSES CHARLES BUJAGA (SUMVE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, upi mpango wa kupitia upya au kupunguza tozo wanazotozwa Wakulima wa choroko kupitia COPRA, AMCOS na Halmashauri ili Wakulima wanufaike.

**118. MHESHIMIWA SALUM KHAMIS SALIM (BUBUBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wakulima wa Mpunga kuzalisha kwa wingi na kuuza nje ya nchi.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**119. MHESHIMIWA ASMA ALI MWINYI (WELEZO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini DIT itafungua Kampasi Shirikishi Zanzibar na Serikali kukamilisha tathmini ya gharama, ratiba na rasilimali zinazohitajika kwa mradi huu.

**WIZARA YA MAJI:**

**120. MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Vijiji vya Kwimba vitapatiwa huduma ya maji.

**121. MHESHIMIWA ZAINAB RASHID KAWAWA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji kutoka Bwawa la Mto Rufiji.

**WIZARA YA UJENZI:**

**122. MHESHIMIWA DKT. LAZARO KILLIAN KOMBA (PERAMIHO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya kutoka Peramiho – Maposeni – Kilagano kwa kiwango cha lami.

## V. HOJA ZA SERIKALI:

### MAAZIMIO:

### WAZIRI WA KILIMO:

Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kimataifa wa Sukari wa Mwaka 1992 *(International Sugar Agreement of 1992).*

### WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Tanzania Kujiunga na Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Usalama wa Angamtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2014 (Mkataba wa Malabo).

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**05 NOVEMBA, 2026** **KATIBU WA BUNGE**